**4R za Dk.Samia zimeponya majeraha**
UK 2

**WHO yaanika mrithi wa Ndugulile**

Kisima Cha Maarifa

# FIKRA PEVU

fikrapevu | @fikrapevu | @fikrapevu

www.fikrapevu.co.tz | ISSN 3456-16 Toleo Na.16 Fikra Pevu Alhamisi Februari 6, 2025 Bei Tsh. 1,000 | Ksh. 100



# Historia imeandikwa

- >> Miaka 48 ya CCM yafana Dodoma
- >> Rais Samia achekelea mafanikio ya serikali yake
- >> Awaonya wana CCM kutowadharau wapinzani

UK 2

## TRA yaanza usajili wafanyabiashara Kariakoo



UK 2

# Dk.Samia anatisha!

- >>Usambazaji umeme sasa wafikia asilimia 52.3
- >>Serikali yasisitiza umeme kufika maeneoya uchimbaji madini

UK 2



# Historia imeandikwa

NA MWANDISHI WETU

CHAMA cha Mapinduzi (CCM)kimehitimisha kwa kishindo sherehe za kuzaliwa kwake kwa Mwenyekiti wake Rais Dk.Samia Suluhu Hassan,kuwaasa wanachama na wafuasi wa chama hicho kutobweteka na mafanikio ya serikali na badala yake wanatakiwa kuendelea kupambana ili kuwatumikia Watanzania.

Akihutubia maelfu ya wananchi waliohudhuria sherehe hizo zilizofanyika uwanja Jamhuri jijini Dodoma,Rais Samia alisema,watanzania wanatakiwa waone thamani ya chama hicho kupewa ridhaa ya kuongoza serikali yao ambapo ni jukumu la wana CCM kujituma katika majukumu yao.

Alisema,CCM ni chama imara chenye mtaji mkubwa wa wanachama ambao wanaofikia milioni 12 pamoja na wapenzi wengi,lakini bado haitoshi kuwafanya wabweteke kuelekea uchaguzi Mkuu.

"Ndugu zangu pamoja na hali hiyo ya kujiamini na kwamba CCM ndio Chama kikubwa na tuna matumaini makubwa kwenye uchaguzi ujao, tusibweteke. Tunatimiza miaka 48 katika mwaka wenye vuguvugu la uchaguzi mkuu nchi, kama nilivyosema katika mkutano mkuu uliopita hivi karibuni tusiruhusu kunyemelewa na kiburi cha kuwabeza wapinzani wetu lakini pia tusiingiwe na pepo la kuwaogopa"

"Tunataka watupime kwa tunachokifanya leo, watuchague kwa sera pamoja na mipango mizuri," alisema Dkt Samia huku akishangiliwa na umati wa Wana CCM pamoja na wapenzi wa chama hicho waliohudhuria sherehe hizo.

Mwenyekiti huyo wa CCM alizishukuru Jumuiya za Chama hicho UVCCM,UWT na Sekretarieti ya chama hicho kwa hamasa na kufanikisha maandalizi ya sherehe hizo.

Dk.Samia aliwataka wanachama wa chama hicho kujiandaa kwa kampeni za Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba huku akiwaondoa hofu dhidi ya wapinzani, lakini bila kuwadharau.

Vilevile katika hotuba yake mwenyekiti huyo ametilia mkazo kuimarisha Jumuiya ya Vijana UVCCM, ambao ameitaja kuwa ndiyo itakayojenga chama imara kwa kuandaa viongozi wajao watakaokiendeleza chama hicho kuendelea kushika hatamu za uongozi.

"Kesho salama ya Chama chetu na Nchi yetu itahakikishwa kwa vijana wetu kujengewa uwezo ndani na nje ya nchi ili waweze kujipanga kitaasisi na waweze kupambana kwa hoja na yeyote mwenye hoja hasi kwetu, lazima umoja wa vijana wa CCM waendelee kuimarishwa kimkakati kwani hawa ni hazina ya chama, lazima wajengewe uwezo, wapikwe kiitikadi na katika mazingira ya dunia ya sasa, hawa wakikuwa ndio wanaoimarisha jumuiya za UWT na Wazazi"

Kuhusu ajira kwa vijana, Dkt Samia alisema,tayari wameanza kuboresha sekta ya elimu wezeshi ambayo inatoa fursa kwa vijana kusomea mafunzo ya ufundi ili waweze kujiajiri pamoja na kuwaajiri wenzao.

Alisema,masuala ya utalii, uchumi wa bluu pamoja na elimu ni miongoni mwa mambo yanayotiliwa mkazo ili kuwakomboa vijana katika tatizo kubwa la ukosefu wa ajira linaloikumba dunia hivi sasa.

Kwa upande wa matumizi ya TEHAMA,mwenyekiti huyo alisisitiza matumizi ya teknolojia hiyo kwa maendeleo, huku akitoa mfano jinsi yeye mwenyewe alivyoweza kuwatumia ujumbe wanachama wengi akiwataka wajitokeze kwenda kupiga kura katika uchaguzi wa serikali za mitaa uliofanyika nchi nzima Agosti mwaka jana na kufanikisha chama chake kushinda kwa kishindo.

Sherehe kama hizo pia zilifanyika katika maeneo mbalimbali nchini, huku Wana CCM wakijipongeza kwa kuwa ni chama imara kinachoendelea kuaminiwa na wananchi na kushika dola kwa miaka mingi.

Awali Makamu Mwenyekiti wa CCM, Mzee Steven Wasirra akizungumza katika sherehe hizo alisema, CCM kinaendelea kuongoza kutokana na kupata ridhaa ya Watanzania, hivyo amewataka wale wanaosema chama hicho kimekaa sana madarakani, waeleze kama kuna ahadi au mipango ya muda ambayo walikaa na kupangiana kutawala kwa zamu.

Alisema,tangu alipochaguliwa kushika nafasi hiyo jana ikifikia siku ya 17, ameshakutana na watu wengi na kupata uhakika wa jinsi CCM ilivyojijengea heshima.

Aidha kupitia sherehe hizo,CCM iliwatambusha rasmi wagombea Urais wake wakiongozwa na Dk.Samia Urais wa Jamhuri ya Muungano na Dk.Hussein Mwinyi kule Visiwani Zanzibar.

Chama hicho kilimtambulisha Mgombea mwenza wa Dk.Samia ambaye ni balozi Dk.Emmanuel Nchimbi lakini pia chama hicho kilimtambulisha Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Steven Wasirra.

# WHO yaanika mrithi wa Ndugulile

Na Mwandishi Wetu

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO) limetangaza uteuzi wa Dk.Chikwe Ihekweazu kama Kaimu Mkurugenzi wa Kanda ya Afrika, huku likiweka wazi kuwa, Mkurugenzi mpya wa Kanda atachaguliwa Mei mwaka huu.

Uteuzi huo unakuja kufuatia kifo cha aliyekuwa Mkurugenzi mteule wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Kanda ya Afrika, Dk Faustine Ndugulile aliyefariki dunia Novemba 27, 2024 nchini India alikokuwa akipatiwa matibabu.

Kufuatia kifo hicho Desemba 2, 2024 Rais wa Tanzania, katika hafla ya kuaga mwili, Samia Suluhu Hassan alisema nafasi ya Dk Ndugulile itaelekezwa kwa Mtanzania mwingine mwenye sifa.

Katika salamu zake, Rais Samia alisema nchi ilimpata mwakilishi: "Wanadamu tunapanga yetu, lakini Mungu anatupangia, Dk Ndugulile ameiweka nchi pazuri lakini Mungu amechukua kilicho chake.

"Tutaingia tena kwenye mashindano tutatafuta Mtanzania mwenye sifa anayeweza kushindana na ulimwengu, tutaingia tena na tutaweka mtu mwenye sifa ileile kutuwakilisha," alisema Rais Samia.

# TRA yaanza usajili wafanyabiashara Kariakoo

Na Mwandishi Wetu

KAMISHNA Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania(TRA) Yusuph Mwenda,na Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, wamewahakikishia wafanyabiashara wa Soko la Kariakoo kuboresha huduma muhimu ikiwemo kuanzisha kanzidata ya wafanyabiashara wote wa eneo hilo.

Hayo yamejiri katika mkutano maalumu uliofanyika jijini Dar es Salaam jana kati ya TRA,Mpogolo,Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Jukwaa la Wafanyabiashara Kariakoo.

Kwa upande wa Kamishna Mkuu wa TRA, Mwenda,alisema kupitia Jumuiya ya Wafanyabiashara Kariakoo, wamewasimika mabalozi wa nyumba kwa nyumba kuwa wasimamizi wa kampeni ya kurasimisha biashara na kuhakikisha watu wanasajiliwa na kupatiwa namba ya mlipakodi (TIN) ili walipe kodi kwa hiari.

Mwenda, amesema mabalozi hao watasaidia kuwepo kwa usawa katika kulipa kodi kwa hiari ambayo itaweka ushindani uliosawa sokoni



# Dk.Samia anatisha!

Na Mwandishi Wetu

NAIBU Waziri wa Nishati,Judith Kapinga amesema kuwa hadi kufikia Januari mwaka huu Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA), imekamilisha upelekaji wa umeme kwenye vijiji vyote 12,318 nchini na kwamba kazi inayofanyika sasa ni kuendelea kusambaza umeme vitongojini.

Mhe. Kapinga ameyasema hayo leo Februari 04, 2025 bungeni jijini Dodoma wakati akijibu swali la la Mbunge wa Viti Maalumu Mhe. Jacquelune Andrew aliyetaka kufahamu ni lini Serikali itamaliza kusambaza umeme kwenye Vitongoji nchini.

"Serikali imepeleka umeme kwenye vitongoji 33,657 kati ya vitongoji 64,359 sawa na asilimia 52.3", Amesema Mhe. Kapinga

Ameongeza kuwa, Vitongoji 30,702 vilivyobaki vitapata umeme kupitia mpango wa miradi ya kusambaza umeme katika vitongoji ambapo tayari Serikali imeshaandaa Mpango wa kupeleka umeme katika vitongoji 20,000 kwa kipindi cha kati ya miaka mitano (5) hadi kumi (10) kuanzia Mwaka wa Fedha 2023/24.

Kapinga ameongeza kuwa, vitongoji 4,020 tayari vipo katika Mpango wa utekelezaji kupitia miradi mbalimbali.

Akijibu swali la Mbunge wa Kilindi,Omar Kigua aliyeuliza ni upi mpango wa Serikali kufikisha umeme kwenye maeneo yote ya uchimbaji wa madini Kilindi, Mhe. Kapinga amesema Wilaya ya Kilindi ina maeneo yapatayo 12 ya uchimbaji wa madini ya dhahabu ambapo kati ya hayo, maeneo 4 tayari yameshapatiwa huduma ya umeme.

Ameyataja maeneo yenye umeme kuwa Maeneo ni Mafulila, Mfyalime/Najim, Masagulu Muheza na Chanungu.Aidha, eneo la Matanda, mkandarasi aitwae DIEYNEM Co. Ltd anaendelea na kazi ya kuweka miundombinu ya umeme na anatarajia kukamilisha kazi hiyo hivi karibuni.

Kapinga amesisitiza kuwa maeneo mengine ya migodi yaliyosalia yatapata umeme kupitia miradi mbalimbali itakayofuata.

Kuhusu utekelezaji wa mradi wa gridi imara katika maeneo ya Mkata na Kilindi Mhe. Kapinga amesema wanaendelea na mazungumzo na Wizara ya Fedha kwa ajili ya kupeleka fedha za kutekeleza mradi huo.

Akijibu swali Mbunge wa Kiteto,Edward Olelekaita aliyetaka kufahamu kauli ya Serikali kutokana na wananchi kuunguza vifaa kwa sababu ya kukatika kwa umeme, Mhe. Kapinga amesema Serikali inao utaratibu wa kuwalinda watumiaji wa umeme kupitia EWURA na kutoa rai kwa mwananchi ambaye amepata athari kushughulikia malalamiko kupitia EWURA.

Akijibu swali la Mbunge wa Iringa,-Jesca Msambatavangu aliyetaka kufahamu ni lini Serikali itaanza kusambaza umeme kwenye mitaa 15 ya kila majimbo ikiwemo Iringa Mjini mtaa wa Mtalagala na Msisima,Kapinga amesema tayari Mkandarasi yupo eneo la kazi na ameshamaliza uhakiki.

Aidha,kwa niaba ya Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati amelielekeza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuja na mkakati wa kuwa na nguzo za chuma ili zikae maeneo ya milimani.

# Mahundi akabidhi mtambo wakucha dhahabu Kyela

Mwandishi Wetu

NAIBU Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Maryprisca Mahundi amekabidhi Mtambo wa kuchakata Dhahabu (Karasha) kwa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) wilayani Kyela

"Lazima tuhakikishe tunasimamia maono yetu,lazima mimi kama kiongozi nisimamie yale maono yakusema twende tukue pamoja nihalikishe kundi kubwa ninaloliwakilisha lazima tukue pamoja"

Akiongea na kundi hilo la Wanawake wa Kyela alisema,kupitia Karasha hilo litakwenda kunyanyua Uchumi wa kundi la Wanawake wilayani humo.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania wilayani Kyela Bi Sesilia Mwakang'ata amempongeza Naibu Waziri Maryprisca Mahundi katika uongozi wake wa miaka minne alijiwekea mipango yake namna ya kuishi na kundi kubwa la wanawake mkoani Mbeya .

"Tunashukuru sana kwa kutupatia mradi huu wa kuchakata dhahabu kwa mikono miwili"alisema Sesilia

# Unafahamu chanzo cha Msongo wa mawazo?

WIKI iliyopita tulizungumzia sehemu ya kwanza ya tatizo la msongo wa mawazo na ufumbuzi wake.Katika mfululizo wa makala hii tuliishia kuzungumzia sababu zinazosababisha msongo wa mawazo.Sababu namba mbili inayosababisha msongo wa mawazo:

2.MATATIZO YA KIFEDHA

Msongo wa mawazo unaweza kusababishwa na matatizo ya kifedha kwa sababu zifuatazo

Ukosefu wa ajira, kudaiwa fedha nyingi sana,kulipwa fedha kidogo sana kwenye ajira au kibarua, kufukuzwa kazi na biashara kuingiza fedha kidogo sana.

Matatizo mengine ni mwenza wako kuiba mali zako na kuziuza kisha akatokomea kusikojulikana, kufilisika, kufilisiwa, kuibiwa, kudhulumiwa, kutapeliwa, kuvamiwa na majambazi,majanga ya asili kama ukame, mafuriko, tetemeko, kimbunga na watu kukopa fedha zako nyingi lakini hawarudishi.

**3.MATATIZO YA KIFAMILIA/MAHUSIANO**

Msongo wa mawazo unaweza kusababishwa na matatizo ya kifamilia/mahusiano kwa vyanzo vifuatavyo:

MAHUSIANO

Vyanzo ni kumfumania mwenza wako, kusalitiwa, kugundua mwenza wako amezaa na mtu mwengine, kugundua mwenza wako ameathirika na ugonjwa usiokuwa na tiba kama ukimwi, kutelekezwa na ujauzito,mwenza wako kutoroka kwenda kwao mara kwa mara,

Mwenza wako kukufokea, kukutukana, kukudhalilisha hadharani, kukuita majina ya udhalilishaji,kutishia muachane mara kwa mara,kukunyima unyumba kila siku, kukupa kashfa za uongo za usaliti kila siku,kupigwa mara kwa mara, kuingiliwa kinguvu, kuingiliwa kinyume na maumbile. Mwenza wako kukubambikia kesi mahakamani,mwenza wako kuvunja mahusiano ghafla, mwenza wako kukata mawasiliano ghafla.

FAMILIA

Ugomvi wa mara kwa mara wa wazazi wako,ugomvi wa ndugu zako wa damu na wazazi wako,kutengwa na familia yako,talaka au kutengana kwa wazazi wako,kuuguza mzazi au wazazi,mzazi kuwa mzee sana au mlemavu.

4.MATATIZO BINAFSI

Unaweza kusumbuliwa na msongo wa mawazo kwa sababu binafsi kama vile

#kujichukia kwa muonekano, kusumbuliwa na ulemavu wa kudumu , kuichukia kazi yako,kuichukia taaluma yako,hofu ya kukosolewa,hofu ya kufa,kuichukia familia yako,kumchukia mwenza wako lakini hajakukosea chochote,

Tishio la usalama wako,tishio la kufungwa gerezani,tishio la kufukuzwa kazi, kukosolewa mara kwa mara kuathirika na ulevi kupindukia, kucheza kamari, kuvuta bangi, kutumia dawa za kulevya,kutumia fedha nyingi sana bila kujizuia.

Nyingine ni kuathirika na kujichua (masterbation),kujiona mzee sana kabla ya umri,kuona umri unazidi kuongezeka bila kupiga hatua yoyote kiuchumi na kifamilia.Kugombana na watu wa karibu mara kwa mara bila sababu zozote za msingi.

**5.KUMBUKUMBU ZENYE KUHUZUNISHA NA MALEZI YA UTOTONI**

**Unaweza kusumbuliw**a na msongo wa mawazo kwa sababu za kumbukumbu mbaya zenye kuhuzunisha kama vile kutekwa nyara,kubakwa, kulawitiwa, vipigo,kupata ajali yenye kusababisha ulemavu wa kudumu,kifo cha ghafla cha mpendwa wako, kusababisha ajali au kifo cha mpendwa wako kwa uzembe.

Kunyang'anywa mali, kufungwa gerezani, kushuhudia mzazi wako anapigwa, kufokewa, kutukanwa,kubamizwa ukutani, kurushiwa mawe, kunyimwa chakula, kufukuzwa nyumbani, kulazwa chooni,kubakwa , kulawitiwa,kuuawa n.k.

Vilevile kumbukumbu zenye kuhuzunisha kama kupigwa, kufokewa, kutukanwa,kudhalilishwa, kunyimwa chakula, kutengwa, kubaguliwa,kufanyiwa uonevu mara kwa mara.

III.MADHARA YA MSONGO WA MAWAZO

Madhara ya msongo wa mawazo ni kuongezeka kwa matatizo ya kiafya, kupitia kipindi kigumu sana kifedha,kutumia dawa za kulevya, pombe kupindukia, kuvuta bangi, kufukuzwa kazi,kufanya uhalifu, kujidhuru au kuwadhuru watu wengine.

UFUMBUZI WAKE

Msongo wa mawazo unaweza kukabiliwa kwa njia zifuatazo

1.KUJUA CHANZO CHA TATIZO HUSIKA

Unaweza kukabiliana na msongo wa mawazo kwa kufahamu chanzo cha tatizo lako na viashiria vya tatizo hilo.Kabla ya kukabiliana na msongo wa mawazo unatakiwa kukabiliana na viashiria vya msongo wa mawazo ambapo ni kupata utulivu wa akili.

Njia za kupata utulivu wa akili ni kama vile mazoezi ya kupumua (Deep breathing exercises, Yawning, Belly breathing) maelezo yake yako kwenye makala za nyuma pamoja na ndani ya kitabu cha JINSI YA KUPONA MAUMIVU MAKALI SANA MOYONI

2.TENGANISHA MATATIZO SEHEMU MBILI

Sehemu ya kwanza kuna matatizo yapo nje ya uwezo ambao hauna uwezo wa kukabiliana nayo kwa mfano hauna uwezo wa kubadilisha tabia ya mtu mwengine,hauna uwezo wa kubadilisha historia yako,hauna uwezo wa kutawala maamuzi ya watu wengine.

Hauna uwezo wa kuzuia watu wengine kufanya makosa,hauna uwezo wa kuzuia wapendwa wako kuugua au kifo kwa sababu ni mambo ambayo yanatokea kwa watu wote ulimwenguni bila kujali juhudi na umakini.

Hauna uwezo wa kuzuia mwenza wako kusaliti ila unaweza kumsamehe au kumuacha kisha uanze upya kutafuta mwenza mwengine.Hauwezi kumridhisha kila mtu haijalishi utaongea nini au kufanya kitu gani.

Matatizo ambayo yapo nje ya uwezo hutumika kujenga uvumilivu, kujifunza kusamehe, kujifunza tabia za watu, kubadilisha malengo au njia za kufikia malengo yako,kujua nguvu zako na madhaifu yako.

Kujua matumizi ya fedha,kupata uzoefu wa kitu fulani,kujua sifa za marafiki,kujua sifa za mwenza sahihi,kujua namna ya kujitetea,kujua namna ya kukabiliana na watu wenye tabia tofauti na za kwako.

3.TUMIA MAUMIVU YAKO KAMA HAMASA

Kwa mfano utotoni ulipitia manyanyaso unaweza kuanzisha kampeni ya kupinga ukatili kwa watoto,kwa mfano ulipitia manyanyaso kazini unaamua kuwa mtetezi wa wafanyakazi wenye kunyanyaswa kazini,kwa mfano ulidhulumiwa mali zako unatumia fursa hiyo kujifunza sheria na unakuwa mtetezi wa wenye kudhulumiwa,

Kama ulipitia ubaguzi shuleni unajifunza kukabiliana na vitendo vya ubaguzi popote uendapo,kwa mfano ulipitia kipindi kigumu sana kifedha unachukua uamuzi wa kujikwamua kifedha,

Kama mwenza wako alikufanyia udhalilishaji kwa sababu alikuwa na fedha nyingi zaidi yako unaamua kujikwamua kifedha kwa maana yale maumivu makali sana moyoni yanakuwa hamasa ya mafanikio badala ya kutaka kutia huruma kwenye jamii.

4.ZINGATIA KWAMBA: MATATIZO HUTOKEA KWA WATU WOTE ULIMWENGUNI

Matatizo hayatakwisha ulimwenguni haijalishi utalia,utacheka,utakata tamaa matatizo yapo palepale.Matatizo hayatazami malengo yako, matatizo hayatazami kipato chako, matatizo hayatazami machozi yako, matatizo hayatazami wewe ni mchamungu au mshirikina, matatizo hayatazami wewe ni muaminifu au msaliti,

Matatizo hayatazami wewe ni mlemavu au upo na viungo kamili, matatizo hayatazami umri wako, matatizo hayatazami familia ambayo umetokea, matatizo hayatazami kiwango cha elimu yako, matatizo hayatazami kama ni mgonjwa au upo na afya.

Matatizo hayatazami muonekano wako, matatizo hayatazami kama huwa unasaidia sana watu au hauna msaada wowote katika jamii, matatizo hayatazami unaishi wapi.Matatizo ni kama mvua ikinyesha inanyesha tu haijalishi unaishi kwenye ghorofa au nyumba ya tope.Ukikata tamaa haiwezi kuzuia mvua kunyesha au kujua kuwaka,ukikasirika kwa hali ya maisha yako haiwezi kuzuia kitu chochote hapa ulimwenguni.

Kama tatizo lako ni kubwa zaidi tunaweza kuwasiliana kwa ajili ya Counselling session na ufafanuzi wa kilichoandikwa hapo juu na utaona mabadiliko na kujisikia nafuu ndani ya muda mfupi baada ya mazungumzo.(Counseling kwa njia ya simu gharama Tshs 30000 , kuonana uso kwa uso Tshs 40000.

**Mawasiliano**
**+255766862579**
**+255622414991**
**Imeandikwa na Psychologist Said Kasege.Temeke,Dar es salaam**





# Donald Trump anaipa somo zito Afrika

RAIS wa Marekani Donald Trump anaendelea kufundisha Dunia maana ya uongozi serious wenye matokeo na kuacha alama.Fikiria mwamba hajamaliza hata mwezi mmoja Ikulu tayari dunia inaona mabadiliko makubwa ya kimkakati ya kisera yakitikisa ulimwengu.

Mwamba ndani ya mwezi mmoja tayari kila mtu duniani amekaa mguu usawa, ni mwendo wa utekelezaji mipango ya kimkakati na mabadiliko makubwa kwa vitendo. Trump anatuonesha tofauti ya viongozi mizigo na viongozi wachapakazi.

Trump anachukizwa na utegemezi wa nchi nyingi za kiafrika. Akili yake haiamini kama tunastahili kuendelea kuwa tegemezi wakati nchi zetu zina rasilimali za kutosha. Kwake msamiati wa Afrika kuendelea kuwa ombaomba ni dhambi asiyotaka kuisikia.

Kwanini tuendelea kuitegemea Marekani kuipatia Afrika Msaada.Je sisi ni raia wa Marekani?Je tunalipa kodi au tozo Marekani?Je tunawafanyia nini cha Maana Marekani tustahili misaada ?Kwa Nchi nyingi za Afrika zina utajiri wa Madini ya aina mbali mbali ,Ardhi ,Bahari ,Maziwa na mito , vivutio vya kitalii ni ujinga kulilia misaada.Huu ndo msimamo wa Trump.

Kuna kitu Trump anatufundisha.Kwa sasa ni ngumu kumuelewa. Siyo siku nyingi somo lake litawaingia Waafrika.Kwake anaamini Mungu ameipa Africa kila kitu labda akili tu ya kujua kutumia vyema rasilimali zetu.

Trump ni Rafiki mwema anatufundisha namna ya kujitegemea na kuachana na misaada yenye Masharti magumu.Trump hajaingia Ikulu kutafuta pesa yeye tayari ni bilionea, lengo lake ni kufanya mabadiliko makubwa na kuimarisha zaidi uchumi wa Marekani na uongozi wake kidunia katika kila nyanja.

Viongozi wengi wa dunia ya tatu wanaingia madarakani na kukaa kusubiri awamu zao ziishe tu ili waingie kwenye historia kwamba nao walikuwa marais, ufisadi unabaki vile vile, umaskini unabaki vile vile, zaidi ni kwamba wanaiba na kutajirisha familia zao ili wakimaliza muda wao wawe na mali za kufanyia anasa



# Vita ya Congo chanzo chake nini?

MASHARIKI mwa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) kumeshuhudiwa mzozo na ukosefu wa utulivu ...Kwa muda usiokuwa chini ya miongo mitatu. Ila katika muongo mmoja uliopita, mapigano makali yamezuka mara kwa mara.

Japo eneo hilo linalojumuisha majimbo ya Ituri, Kivu kusini na Kivu Kaskazini yana jumla ya makundi ya wapiganaji zaidi ya 129, kundi la waasi la M23, ambalo ndilo kuu lililobuniwa baada ya makubaliano ya Machi 23 ya kutafuta amani imekuwa na historia ya machafuko.

Pamoja na sababu za kihistoria, mashindano ya kikanda, na machafuko ya ndani, hali hiyo kwa mara nyingine tena inavuta hisia za kikanda na za kimataifa.

Kundi la M23 ni nini na lilianza vipi?Huwezi kuzungumzia M23 bila kuangazia historia ya jamii ya Watutsi katika eneo la mashairiki mwa Kongo, na ambao pia wako nchini Rwanda.

Makundi mbalimbali yalibuniwa ili kutetea maslahi ya jamii ya watutsi katika eneo hilo. Mwaka 2006 CNDP (National Congress for the Defence of the People) iliundwa na viongozi wa Watutsi wa Congo mashariki. Ilikuja kutokana na kuongezeka kwa mvutano wa kikabila kati ya Watutsi na makundi mengine, hasa baada ya Mauaji ya Kimbari ya Rwanda na mgogoro wa wakimbizi nchini Kongo.

Kundi la waasi la RCD, ambalo lilikuwa limedhibiti eneo hilo, lilikatishwa tamaa na mchakato wa amani na serikali ya Kabila, wakihofia kupoteza mamlaka.

Wakiongozwa na Laurent Nkunda, CNDP ililenga kuwalinda raia wa Kitutsi dhidi ya mashambulizi ya makundi ya wanamgambo wa Kihutu na kupata uwakilishi bora wa kisiasa kwa Watutsi katika serikali ya Kongo.

Kuundwa kwa CNDP kwa kiasi kikubwa kulitokana na kushindwa kwa mchakato wa amani na kutozingatiwa kwa mahitaji na usalama wa jamii ya Watutsi.Vita vya Kwanza na vya Pili vya Kongo (1996-2003): Nchi jirani ziliingilia kati mzozo wa DRC, na kuunda mtandao tata wa ushirikiano na ushindani.

Makundi yenye Silaha: Makundi kama vile CNDP (Congress of the National

Chimbuko la M23C-NDP, kikiongozwa na Laurent Nkunda, awali kiliundwa ili kulinda jamii za Watutsi lakini lilijulikana kwa ukiukwaji wa haki za binadamu na biashara haramu.

Mnamo 2009, makubaliano ya amani yalitaka kuunganisha vikosi vya CNDP katika jeshi la Kongo, lakini mvutano uliendelea, na kusababisha kuundwa kwa M23 mnamo 2012. Kundi hilo lilipewa jina baada ya makubaliano ya amani ya Machi 23, 2009 ambayo yaliahidi kuunganishwa kwa wapiganaji wa CNDP katika jeshi la Kongo na kutambua mrengo wao wa kisiasa.

Hata hivyo, kikundi cha CNDP kilidai kuwa makubaliano hayo hayakutekelezwa vyema na kuzaliwa kwa M23 ili kushinikiza madai yao.M23 inadai kulinda jamii za Watutsi na wanaozungumza Kinyarwanda nchini DRC, ikitaja vitisho kutoka kwa wanamgambo wa Kihutu na kushindwa kwa serikali kulinda usalama wao.Licha ya madai hayo, kundi hilo limekuwa likishutumiwa kwa ukiukaji mkubwa wa haki za binadamu, ikiwemo mashambulizi dhidi ya raia.

Uwezo wa kijeshi wa M23

Kufikia Januari 2025, makadirio yanaonyesha kuwa vikosi vya M23 vina wapiganaji kati ya 3,000 na 4,000. Zaidi ya hayo, ripoti kutoka Umoja wa mataifa zinaonyesha kuwa wanajeshi wa Rwanda wanaunga mkono operesheni za M23, ingawa Rwanda imekuwa ikikanusha vikali madai ya kuhusika kwake.

Aidhaa Rwanda imeendeleza madai kwamba kundi la wapiganaji la FDRL ambalo lilitajwa kuhusika katika vita vya kimbari vya 1994, lilikimbilia DRC na linatumiwa na taifa hilo kuendeleza muaji ya kimbari ndani ya Mashariki mwa DRC, jambo ambalo Kinshasa imekanusha vikali pia.



# Unafahamu asili ya mgogoro wa Rwanda na Congo?

USIKU wa Machi 16,1996 viongozi wa Rwanda, Uganda, Sudani Kusini na Ethiopia pamoja na kiongozi wa AFDL Laulent kabila walisaini "Makubaliano ya mkataba wa Lemera".

Mkataba huu ulikuwa na shabaha ya kugawa nchi hiyo kubwa mikononi mwa Marekani kupitia usimamizi wa Rwanda, Uganda, Sudani kusini na Ethiopia, huku Kenya na Tanzania wakiwa ndio wenyeviti wa kuinjinia mkataba huo wa lemela.

Japo baadae Tanzania ilijitoa kuunga mkono kuigawanya Kongo baadala yake ikaunga mkono msimamo wa Laurent Kabila katika kukataa kuutekeleza mkataba wa lemela, ambao kupitia mkataba huo ilizalishwa operation maalum iliyoitwa "Operation Banyamrenge".

Operation hii ililenga kumuondosha madarakani Mobutu, kiongozi wa muda mrefu wa Kongo na kibaraka wa Marekani ambao mpaka kipindi hicho walikuwa tayari wamemchoka kutokana na mabadiliko ya siasa za dunia.

Katika Makubaliano hayo yalio fanywa kati ya Laurent Desire Kabila na mataifa hayo huku Kabila akiwa kama kiongozi wa chama cha "kuikomboa Kongo" aliyekuwa akitaka kuondosha utawala wa dikteta Mobutu Sese Seko alipewa masharti ambayo yalianishwa kwenye mkataba wa Lemera.

Ambapo moja ya masharti ilikuwa ni kishirikina na wapiganaji wa Kinyarwanda kutoka Rwanda, Uganda na watutsi walio kuwa na makazi mashariki mwa Kongo, na baadae ya mapigano atoe sehemu ya ardhi mashariki mwa Kongo kama shukrani kwa Rwanda na Uganda huku akiruhusu usalama wa taifa hilo kuwa mikononi mwao.

Makubaliano hayo yalifanyika kwenye vilima vya Lemera vilivyoko Kivu ya Kusini katika mji wa Uvira na kujulikana kwa jina hilo, la "mkataba wa lemera" makubaliano hayo yalitaka Kabila, baada ya kuwa rais wa Kongo, aruhusu mikoa miwili ya Kivu Kaskazini na Kusini kuwa makazi ya Wanyarwanda wa kabila la Kitutsi.

Laurent Desire Kabila alikuwa tayari amechoka Kwa takribani miaka 20 ya kupambana na utawala wa Mobutu Sese Seko hivyo aliona ni bora kukubali masharti yeyote yale ya mkataba ili tu aweze kumtoa Mobutu madarakani.

Ukweli ni kwamba pamoja na mkataba huo lakini bado Laurent Kabila alikuwa na hesabu zake kichwani ambazo alizipania kuwageuka baada ya ushindi wa kumfurusha Mobutu ikulu ya Palace de la ñatíona iliyopo Kinshasa, na inadaiwa kuwa baadhi ya mikakati baada ya ushindi aliwashirikisha TISS (shirika la kijasusi la Tanzania) ili wampe baraka za kuwageuka Rwanda na Uganda.

Baada ya makataba huo kusainiwa, ukainjinia operation maalum iliyopewa jina la "Operation Banyamrenge" operation hii ilisukwa vyema mjini Kigali, Rwanda kwa kuundwa kikundi cha wapiganaji waliojiita "wapinzani wa dikiteta Mobutu."

Hawa walikuwa Wakongomani na Wanyarwanda kutoka Rwanda na wengine waliokuwa wakiishi mkoa wa Kivu Kusini, Mashariki mwa Kongo. Katika kundi hilo alikuwemo Mkongomani, Jenerali Andre Kisasi Ngando, askari





# Samia ndiye Rais,Wapinzani wajipange kwa ubunge,udiwani

Na Mwandishi Wetu

MANENO haya yanaweza kuwa na maumivu makubwa sana kwa upinzani wa Nchi hii na kuonyesha pengine kuwakatisha Tamaa. Lakini huo ndio ukweli wenyewe na ndio uhalisia wenyewe wa Mambo .



Kwamba mpaka sasa Rais Na makamu wa Rais watakao Ongoza Taifa letu kwa kipindi cha Miaka mitano ijayo mpaka 2030 tayari wanafahamika na tayari DUNIA nzima inawafahamu. Kuwa Ni Mheshimiwa Rais Daktari Mama Samia Suluhu Hasssan na Makamu wake ni Balozi Daktari Emmanueli Nchimbi.

Hata watanzania kwa sasa wanajua uchaguzi wa Urais Umekwisha na kuishia siku ile CCM kupitia mkutano mkuu wake maalumu ulipopitisha majina hayo na leo kutambulishwa Rasmi katika siku ya kusherehekea na kuadhimisha miaka 48 ya CCM tangia kuzaliwa kwake.

Hii ni kwa kuwa ni CCM pekee ndiyo chama chenye uwezo wa kutoa mtu mwenye uwezo na sifa za kuongoza Taifa letu. Ni CCM pekee itakayoendelea kutoa RAIS na Makamu wa Rais wa Taifa letu Mpaka Mwisho wa Dunia. Ni CCM pekee ndio itakayoendelea kutoa Dira na muelekeo wa Taifa letu .

Kwa hiyo ni muhimu vyama vya Upinzani vikatumia muda huu mfupi uliobakia kuandaa wagombea bora na wanaokubalika na kuuzika kwa wananchi katika nafasi za ubunge na udiwani. Huu ni muda wa kuweka mipango, mikakati ya kuandaa rasilimali watu na Fedha kwa ajili ya uchaguzi ujao.

Ni muda wa kuandaa timu nzuri na yenye kusheheni watu wenye ushawishi,nguvu , kukubalika na wenye uwezo mzuri wa kujenga hoja watakao tumika kunadi wagombea ubunge na udiwani.



> Kwamba mpaka sasa Rais Na makamu wa Rais watakao Ongoza Taifa letu kwa kipindi cha Miaka mitano ijayo mpaka 2030 tayari wanafahamika na tayari DUNIA nzima inawafahamu. Kuwa Ni Mheshimiwa Rais Daktari Mama Samia Suluhu Hasssan na Makamu wake ni Balozi Dak

Huu ni muda wa kuweka mipango ya kisayansi na yenye utafiti wa kisayansi ya juu ya wapi na mahali gani chama kiweke nguvu za kutosha katika kuhakikisha kuwa maeneo hayo kitafanikiwa kupata wabunge na madiwani wa kutosha .

Ni muda wa kuangalia wapi chama kina nguvu na ngome za kihistoria na namna gani ya kuendeleza na kutumia historia hiyo kupata ushindi kwa kuleta watu wenye sifa na ushawishi. Vyama vya Upinzani ni lazima visahau kabisa na kufuta kabisa habari za Urais kwa sababu huko watakuwa wanapoteza muda na rasilimali tu bila sababu ya Msingi bila kupata matunda.Uchaguzi ni hesabu na Siasa ni sayansi na sayansi ina kanuni zake.

# MAAMUZI YA TRUMP YATUFUNGUE MACHO HARAKA



NA MWANDISHI WETU

UTU wetu na thamani yetu, ilishuka miaka mingi, baada ya kuukumbatia ulemavu wa kusaidiwa. Tukubaliane waafrica, kuna ujinga fulani tumeushikilia, tungekuwa watu wa kuendelea kupitia misaada, tungeshatoka hapa tulipo.

Ukweli ni kwamba, misaada mingi ya magharibi haijawasaidia walengwa wa misaada hiyo zaidi ya kuishia mifukoni mwa watu wachache. Nitamshangaa Prof.Anna Tibaijuka, kuulizia Ukimwi ulianzia wapi?.Ukimwi ulianzia Marekani,Kama ulianzia huko, ni kwa nini Umeua na kuteketeza waafrica wengi zaidi??.

Motive ya kutengeneza,hivi virusi ilikuwa ni nini?.

Ukiisoma, na kuielewa Sayansi ya Kirusi kinavyoingia,kuathiri Chembe hai ya kinga ambayo ni ( Commander in chief), inayotoa amri, kwa chembei kinga nyingine, Lazima ukubaliane nami kuwa, maarifa ya binadamu ya " Genetic engineering yalifanya kazi. Dunia ina mengi ya kushangaza, Ngoja tujadiri tutawasaidiaje ndugu zetu wanaohitaji dawa hizi.

1) Kwa waafrica wote hii ni agenda yetu sote.a) Tu mobilise Resources,zetu tuwe na ushirika na wenye kupenda ushirika nasi, tujenge viwanda vyetu vya madawa, hata ikibidi kuwapeleka wana wa kiume na wa kike wa kitanzania, Kenya na nchi nyingine kupata maarifa ya juu zaidi ya kinga mwili( immunology).

b) Kila nchi inaweza kubeba jukumu moja moja, wakati Kenya wana tengeneza chanjo, sisi tujenge viwanda vya ARV.

2) Tuweke nguvu kwenye kukinga zaidi.a) Panaweza kuwa na vipimo vya kucheck kabla watu hawajaingiliana.b) Tutengeneze viwanda vya kuzalisha Condom nyingi.

C) Mtu anposhtuka kayatimba, basi guest zote ziwe na dawa za kuzuia kirusi hicho kusambaa( Post exposure prophylaxis).

d) Ngono duniani kote baadhi ya maeneo imekuwa ni commodity, basi kuwe na Priority kwenye nchi za kusaidia makundi yaliyoathirika kiuchumi, wapewe mikopo nafuu( serving disadvantaged societies),Ili ku shift equilibrium ya biashara ya ngono, kuja kwenye biashara nyingine.

3) 1,2, hapo juu zinaweza ku apply kama long term plan, short term plan ni kama hizi.a) Tupunguze matumizi.

Badala ya magari ya mil 600, tununue magari ya mil 60!, b) Tuwe na mfuko wa Taifa wa Ukimwi i) 10% ya mauzo ya kodi yaende kwenye mfuko huu.

ii)Tuhamasishe matumize ya Teleconference, badala ya kulazimisha watu kusafiri kwa kuchoma mafuta ya petrol kwa ma V8 ili tuwe na hela ya emergency kwa ajili ya mfuko huu, badala ya kuitumia kununulia mafuta ya magari.

iii) 7% ya mapato ya mashindano yote kwenye mpira iende kwenye mfuko wa Taifa wa Ukimwi. Ninajaribu kuonyesha tu kuwa, hili tatizo liko ndani ya uwezo wetu!, Trump kutunyima misaada, ni NIA njema, ya kutaka tushtuke, tutumie raslimali zetu kwa faida ya watu wetu na si vikundi vya watu.

**TUKATAE ULEMAVU WA KUSAIDIWA.**

**Isaya.**



# Congo DRC ina laana ya utajiri?



Na Mwandishi Wetu

ENEO la Kivu ni eneo la kimkakati sana na mabepari wote duniani wanalitolea macho kutokana na utajiri wake.Kivu ina madini ya Coltan ambayo yanatumika kutengeneza simu na laptop. 80% ya coltan yote duniani inatoka Congo (unaweza kugoogle kama huamini). Yani kwa kifupi bila Congo hakuna smartphones wala laptop duniani.

Kivu pia kuna madini ya tin yanayotumika kutengenezea solder za kuchomelea vifaa vya kielektroniki kama radio,TV,simu,nk.Kuna madini ya Tungsten yanayotumika kutengenezea silaha.

Na pia kuna Cobalt inayotumika kutengeneza betri mbalimbali zikiwemo za magari. Kama haitoshi Kivu kuna dhahabu nyingi mno. Eneo la Kivu ni eneo lenye dhahabu nyingi zaidi duniani ambayo bado haijachimbwa (The most unexplored gold site globally).

Kagame aliona fursa. Wakati huo Rwanda ilikuwa imetoka kwenye vita na machafuko ya muda mrefu. Akataka rasilimali za jirani. Lakini atazipataje wakati yeye na Mobutu hawaelewani? Akaamua kumuunga mkono mzee Laurent Kabila.

Lakini akaweka masharti.Nikikusaidia kumng'oa Mobutu, eneo la Kivu Kusini,lenye Watutsi wengi (Banyamulenge),litajitenga na Congo na kuwa nchi inayojitegemea.

Alishapiga hesabu za mbali za kuifanya Kivu kuwa sehemu ya Rwanda baada ya kujitenga DRC. Kabila akasema poa tu. Ashapigana miaka 30 msituni bila mafanikio? Sasa kapata "kamsereko" ka kwenda Ikulu akatae? Kagame nyuma yake walikuwepo Ufaransa na Uingereza akasema twende kwa maandishi. Mkataba ukasainiwa mji mdogo wa Lemera, Kivu Kusini. AFDL ikapewa support ya silaha na pesa, ikaamsha dude kupigana na majeshi ya serikali (FARDC).

Wakati Mobutu anajaribu kupambana na AFDL, vikaibuka vikundi vingine vya waasi zaidi ya 40 kupigana na majeshi ya serikali. Vita ikiwa imepamba moto, Rwanda ikajitosa rasmi kupigana na serikali ya Mobutu kwa kisingizio cha kuwatafuta wanamgambo wa Intarahamwe waliokimbilia Congo.

Uganda nayo ikaingiza jeshi kuwatafuta waasi wa LRA. Mobutu kaona "nini cha kufia" akadaka chopa akatokomea zake Moroco. Kesho yake Mei 17, 1997, Laurent Kabila akatangazwa Rais mpya wa Congo. Vita hii ikabatizwa jina vita vya kwanza vya Congo (1996-1997).

# Amani yetu imeshikiliwa na CCM imara



Na Mwandishi Wetu

**UIMARA na umadhubuti wa Chama cha Mapinduzi(CCM) chini ya Mwenyekiti wa chama hicho Dk.Samia Suluhu Hassan,ndiyo hasa msingi mkuu wa amani, umoja na mshikamano miongoni mwa Watanzania.**

CCM ndicho chama kilichobeba hatma, matumaini na mustakabali mwema, wa uhakika na salama wa umoja, amani na utulivu wa waTanzania.

Kukubalika na kuaminika kwa sera na mipango mikakati ya maendeleo kumewaunganisha Watanzania, kuwaleta pamoja na kua kitu kimoja. Ama kwa hakika bila CCM madhubuti, nchi itayumba.

Nia na dhamira njema za viongozi waandamizi wa chama na serikali, hasa kiongozi mkuu wa nchi Dr.Samia Suluhu Hassan, vimeendelea kuliunganisha taifa, kuifungua nchi miongoni mwa mataifa ya ulimwengu na kuifanya Tanzania madhubuti zaidi, inayoaminika na kuheshimika ndani na nje ya mipaka ya Tanzania kwa kiwango cha juu sana.


Tunapoelekea uchaguzi mkuu 2025, ni muhimu sana wananchi wote, kufahamu na kuelewa kwamba, ushindi wa kishindo wa CCM, ni ushindi wa wananchi na waTanzania wote, dhidi ya vibaraka wa mabwenyenye ya magharibi, wenye nia ovu binafsi za kutugawanya kwa maslahi yao binafsi.

Kama Taifa inafaa kuungana na tuendelee kuiamini CCM na kuipa nafasi zaidi ya kuongoza, ili hatimae tuendelee kufurahia matunda ya dhamira na nia njema ya Rais Dr.Samia Suluhu Hassan katika kuulinda umoja wetu, na kwa gharama yoyote ile kuitunza amani na utangamano miongoni mwa waTanzania.

Mungu Ibariki Tanzania.



# Wanawake 100 wabakwa na kuchomwa wakiwa hai Congo



**ZAIDI ya wafungwa 100 wa kike walibakwa na kisha kuchomwa moto wakiwa hai wakati wafungwa walipotoroka jela katika mji wa Goma nchini Congo, kulingana na UN.**

Mamia ya wafungwa walitoroka katika gereza la Munzenze Jumatatu iliyopita, baada ya wapiganaji wa kundi la waasi la M23 kuanza kuuteka mji huo.

Kati ya wanawake 165 na 167 walivamiwa na kunyanyaswa na wafungwa wa kiume walipovunja gereza, hati ya ndani ya Umoja wa Mataifa iliyoonekana na BBC inasema.

Ripoti hiyo inaeleza kuwa wengi wa wanawake hao waliuawa baada ya wafungwa hao kuchoma moto gereza hilo.

Goma, jiji kubwa lenye zaidi ya watu milioni moja, lilitekwa baada ya kundi la M23 linaloungwa mkono na Rwanda kuingia na kuteka eneo la mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.Jiji hilo lilikumbwa na machafuko, huku miili ikiwa imetapakaa mitaani na makombora yakiripotiwa kuonekana juu ya nyumba za makazi.



Picha za jela kuvunjwa za wiki iliyopita zilionyesha watu wakitoroka kutoka kwa jengo hilo huku moshi ukiendelea kupaa kwa nyuma.Milio ya risasi pia ilisikika.Katika video tofauti, watu wanaoaminika kuwa wafungwa waliotoroka, walionekana wakiwa wamewasili katika mitaa ya Goma.

Zaidi ya watu 2,000 waliuawa wakati waasi wa M23 wakikabiliana na wanajeshi wa Congo na washirika wao, serikali ya DR Congo imesema.Umoja wa Mataifa unasema takriban watu 900 waliuawa na karibu 3,000 kujeruhiwa.Haikuwa wazi kwa nini idadi ya vifo vya Umoja wa Mataifa na DR Congo inatofautiana.

# Mpango wa Trump Gaza utaonekana kuwaukiukaji wa sheria za kimataifa



**WAKATI Rais wa Marekani Donald Trump alipoanza kuzungumza kuhusu Gaza siku 10 zilizopita kama eneo linalohitaji kuangaziwa, akitoa wito wa "kusafishwa eneo zima", haikuwa wazi ni kiasi gani alimaanisha kwa kutoa kauli hii.**

Lakini kuelekea kwenye ziara ya Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu, akizungumza kabla ya mkutano na waandishi wa habari, ni wazi sasa yuko makini sana kuhusu mapendekezo yake.

Walifikia msimamo wa pamoja zaidi uliowekwa na Marekani kuhusu Israeli na Wapalestina katika historia ya hivi karibuni ya mzozo; na itaonekana kama kukiuka sheria za kimataifa. Pamoja na jinsi tangazo hilo litakavyochukuliwa na watu wa kawaida, linaweza pia kuwa na athari kubwa katika mchakato wa haraka wa kusitisha mapigano na kuwaachilia mateka.

Trump na maafisa wake wanaandaa wito kama anavyoita kwa lugha yake - "kuwapatia mwanzo mpya" Wapalestina wote nje ya Gaza kama ishara ya kibinadamu, wakisema hakuna mbadala wao kwa sababu Gaza ni "mahali palipobomolewa".

Chini ya sheria za kimataifa, majaribio ya kuhamisha watu kwa nguvu yamepigwa marufuku kabisa, na Wapalestina na mataifa ya Kiarabu wataona hili kama pendekezo la wazi linalolenga kufukuzwa kwao na Wapalestina katika ardhi yao.

Ndiyo maana viongozi wa Kiarabu tayari wamekataa kabisa mawazo yake, yaliyotolewa mara kwa mara katika siku 10 zilizopita,akipendekeza Misri na Jordan kuwa zinaweza "kuwachukua" Wapalestina kutoka Gaza.

Katika taarifa yake ya Jumamosi, Misri, Saudi Arabia, Umoja wa Falme za Kiarabu, Qatar, Mamlaka ya Palestina na Jumuiya ya Nchi za Kiarabu zilisema kwamba hatua hiyo inaweza "kuhatarisha uthabiti wa eneo hilo, hatari ya kuongeza mzozo zaidi, na kudhoofisha matarajio ya amani na kuishi pamoja miongoni mwa watu wake".

mrefu imekuwa shauku ya wazalendo wenye msimamo mkali huko Israeli kuwaondoa Wapalestina katika maeneo wanayokaa na kupanua makazi ya Wayahudi katika maeneo yao.

Tangu mashambulizi ya tarehe 7 Oktoba 2023 dhidi ya Israel, makundi haya - viongozi ambao wamekuwa sehemu ya muungano wa Netanyahu - wamedai vita dhidi ya Hamas kuendelea kwa muda usiojulikana, wakiapa kuanzisha upya makaazi ya Waisraeli katika Ukanda wa Gaza. Wameendelea na wito wao na kupinga makubaliano ya sasa ya kusitisha mapigano na kuachiliwa kwa mateka.

Katika mkutano wake na waandishi wa habari katika Ikulu ya White House na Waziri Mkuu wa Israel, Trump alienda mbali zaidi hata kuliko wito wake wa hivi karibuni uliokua ukitaka Wapalestina wa Gaza "wahamishwe" hadi Misri na Jordan, akisema kwamba Marekani italichukua eneo hilo na kulijenga upya.

Alipoulizwa ikiwa Wapalestina wataruhusiwa kurejea, alisema "watu wataishi huko, akisema itakuwa "mahali pa kimataifa,ambapo hapakutazamiwa", kabla ya kuongeza "Wapalestina pia".

Mjumbe wake wa Mashariki ya Kati Steve Witkoff mapema siku hiyo alitoa muhtasari kuhusu pendekezo hilo, akisema kuhusu Trump "jamaa huyu anaelewa kuhusu makazi".

Trump alisema itakuwa "eneo la kuvutia Mashariki ya Kati".Alipoulizwa iwapo wanajeshi wa Marekani watahusika katika kutwaa Gaza, Bw Trump alisema "tutafanya kinachohitajika".

Mapendekezo yake yanafikia mageuzi makubwa zaidi katika msimamo wa Marekani katika eneo hilo tangu kuundwa kwa taifa la Israel mwaka 1948 na vita vya 1967, ambavyo vilishuhudia kuanza kwa utawala wa kijeshi wa Israel katika ardhi hiyo ikiwemo Ukanda wa Gaza.

Gaza ilikuwa tayari makazi ya Wapalestina waliokimbia au kulazimishwa kutoka makwao katika vita vilivyochangia kuimarika kwa Israeli.Wao na vizazi vyao wanaunda idadi kubwa ya wakazi wa Gaza hadi leo.

Mapendekezo ya Trump, yakipitishwa kuwa sheria yangehusisha idadi hiyo ya watu, ambayo sasa ni zaidi ya watu milioni mbili, wanaolazimishwa kwingineko katika ulimwengu wa Kiarabu au hata kwingineko, anasema Trump, "kupata makazi upya ... ya kudumu".

Mapendekezo hayo yatafutilia mbali uwezekano wa suluhu ya baadaye ya serikali mbili kwa maana yoyote ile ya kawaida na yatakataliwa kimsingi na Wapalestina na ulimwengu wa Kiarabu kama mpango wa kuwaondoa.

Sehemu kubwa ya kambi ya kisiasa ya Netanyahu na vuguvugu la walowezi lenye msimamo mkali nchini Israel litatetea kauli ya Rais Trump, wakiyaona kama utimilifu wa hatua kama Netanyahu anavyoiweka kukomesha "Gaza kuwa tishio kwa Israeli".

Kwa Wapalestina wa kawaida, itakuwa sawa na kitendo cha adhabu ya pamoja.



# DAVID BECKHAM ALIJITENGENEZA, AKAJIUMBA KATIKA SOKA



'BRAND Like David Beckham'! Ni msemo ambayo ulikuwa maarufu mwanzoni mwa miaka ya 2000 hasa kwa mashabiki wa soka. Walikuwa na maana ya kusema hivyo.

Huyu David Bechkam alizaliwa Mei 2, 1975 akiwa mtoto wa pili wa Sandra Georgina na baba yake Edward Alan Bechkam. Beckham alizaliwa katika sehemu ya London Masharik inayoitwa Leytostone, Alicheza soka tangu umri mdogo.

'Samaki mkunje angali mbichi', ndivyo wasemavyo Waswahili huyu David Beckham ndiye samaki aliyekunjwa na Sir Alex Ferguson tangu mwaka 1991 alipojiunga na kikosi cha Manchester United akiwa na umri wa miaka 16 tu.

Beckham alikuwa ni mmoja kati ya wachezaji pendwa katika kikosi cha Manchester United chini ya Sir Alex ferguson kwani alimlea akiwa tangu mtoto.

Kipindi cha Sir Alex ndipo kilipozaliwa kizazi cha 'Class of 92', darasa lililoundwa na vijana kama Ryan Giggs, Roy Keane, Phil Neville, Gary Neville na Paul Scholes.

David Bckham ni bishoo wa Uingereza, aliyejipatia pesa nyingi na umaarufu duniani kote kupitia kipaji chake cha soka, huyu ni fundi wa kupiga mipira mirefu na ile ya freekick (Deadball Specialist).

'Band Like David Bechkam' sio msemo mgeni katika masikio ya wapenzi na wanazi wa Manchester United na timu ya taifa ya England, hii ni kwa sababu ya namna anavyoinama wakati akiwa anataka kupiga mpira huo wa adhabu unaopelekea kuingia nyavuni.

David Beckham aliwahi kumgomea Sir Ferguson kwenye suala la kusaini mkataba mpya ili tu ajue hatima na stahiki zake juu ya picha zilizobandikwa kila kona ya Uwanja wa Old Trafford, hapo ndipo namna ya kuji brand ilip anzia na kuanza kuona namna anavyoweza kujipatia pesa.

Huyu David Beckham amezaliwa na kukuta wazazi wake ni mashabiki lialia na wa kutupwa wa Manchester United, kiasi cha kuweza kuzikata kilomita 320 kwenda kuangalia mechi za nyumbani za timu hiyo.

Beckham aliipenda Manchester United mpaka aliwahi kunukuliwa wakati akiwa mdogo akisema, anataka kuja kuwa mchezaji wa timu hiyo.

Ndoto zinakuwa kweli, maana hata maana hata maisha yake ya soka la kulipwa yalianza Manchesyer United akiwa na umri wa miaka 16 na kufanikiwa kushinda taji la Ligi Kuu mara 6, FA mara 2, Ngao ya Jamii mara 2 na Ligi ya Mabingwa Ulaya mara 1.

David Beckham ni mmoja kati ya wachezaji wenye kipaji kikubwa ma baadaye aliamua kutimka na kwenda zake Real Madrid huko Hispania.

Japo taarifa za ndani zaidi zinasema David Beckham alipoanza kukunja mkwanja mrefu hapo Manchester United ndipo mambo yalipobadilika, kwani alianza kuvimba kama wasemavyo vijana wa Kizimkazi, alishawahi kwenda mazoezini na chopa (helikopta) huku akiwa amechelewa.

Pia alishawahi kuvaa rebon kichwani akashindwa kufunga goli baada ya ile rebon kumfunika macho hivyo na vingine vingi ni baadhi ya vitendo ambavyo vilimfanya Sir Alex Fergerson kumuuza kwenda Real Madrid.

David Beckham alicheza madrid kwa misimu minne tu na akafanikiwa kutwaa taji la La Liga na kupelekwa LA Galaxy Marekani kisha kwa mkopo Italia ndani ya AC Milan na kuweka rekodi ya kuwa mchezaji wa kwanza wa Uingereza kucheza mechi 100 za Ligi ya Mabingwa Ulaya

Wakati wa maisha yake ya soka miaka 20, alishinda mataji 19 makubwa kwa klabu na alionekana katika michezo 115 kwa timu England. Mnamo 2004, Pele alimtaja Beckham kuwa mmoja wa wachezaji 100 wakubwa walio hai

Akiwa Real, Beckham alijiunga na Ronaldo, Zidane, Figo, na Ra□l katika kikosi kinachojulikana kama Galácticos. Kwa talanta zote zilizoonyeshwa, ingawa, Real ilijitahidi kushinda taji lolote katika misimu mitatu ya kwanza ya Beckham na klabu. Licha ya ukosefu huu wa mafanikio ya timu, Beckham alikuwa akicheza vyema, na aliongoza La Liga kwa kusaidia katika 2005.

Katika hatua ya kimataifa, Beckham alikuwa na majanga yake kwani kwenye fainali za Kombe la Dunia la 1998, katika mechi ya hatua ya 16 bora dhidi ya Argentina, Beckham alitolewa nje kwa kadi nyekundu kwa kumpiga teke Diego Simeone akiwa amelala uwanjani.

England hatimaye ilipoteza mechi hiyo kwa mikwaju ya penalti, na Beckham akawa mlengwa mkuu wa dhuluma na mashabiki na vyombo vya habari.

FIKRAPEVU
MICHEZO
JUMATANO FEBRUARI 6, 2025

# Yanga yapiga mtu 6-1




## >> Clement Mzize,Dube kila mmoja atupia mara mbili

Na Mwandishi Wetu

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara,Yanga jana waliibuka na ushindi wa mabao 6-1 dhidi ya KenGold mchezo uliopigwa uwanja wa KMC jijini Dar es Salaam.

Ushindi huo umeiwezesha Yanga kurudi kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara na kuwashusha nafasi ya pili mahasimu wao jadi kisoka Simba kwa tofauti ya alama moja.

Katika mchezo huo mabao ya Yanga yalifungwa na Mzize mawili,Dube mawili na mengine yakiwekwa wavuni na Duke Abuya na Pacome Zouzoua.

Mshambuliaji wa Yanga, Prince Dube amefunga bao la kwanza na tano dakika ya 2 na 46, Clement Mzize amepata bao la pili na nne dakika ya 6 ya 42 pasi kutoka kwa Stephen Aziz Ki.

Kiungo Mshambuliaji Pacome Zouzoua amepata bao la 3 dakika ya 39 pasi kutoka kwa Dube, Duke Abuya ameipatia bao la sita dakika ya 85 akiunganisha pasi ya Kennedy Musonda.

Bao la Kwanza la Kengold limefungwa na Selemani Rashid dakika ya 86 baada ya kupiga shuti kutoa kati ya uwanja na kipa wa Yanga, Djigui Diarra kumsinda mpira na kuingia nyavuni.

# Mfuko Maendeleo ya michezo kuzibeba timu za Taifa

Na Mohsin Juma

SERIKALI imeanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Michezo (Sports Development Fund) kwa ajili ya uwezeshaji wa timu za Taifa kufanya vizuri katika mashindano mbalimbali ya kimataifa, uibuaji wa vipaji vya wanamichezo, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya michezo, kulipa mshahara wa kocha wa timu ya Taifa ya mpira wa miguu (Taifa Stars), pamoja na kuwajengea uwezo wa utawala bora viongozi wa vyama na mashirikisho ya michezo nchini.

Mfuko huu unategemea chanzo kikuu cha michezo ya kubashiri matokeo ya michezo, ambapo Serikali ilipitisha sheria kuwa asilimia 5 ya makusanyo ya michezo ya kubashiri (Sports Betting) ielekezwe kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Michezo.

Kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2021/2022, Serikali imetoa jumla ya Shilingi bilioni tisa Milioni Sita Hamsini na Mbili Elfu na mia nane thelathini na mbili (9,006,052,832).

Fedha hizo zimeleta mafanikio katika sekta ya michezo nchini ikiwa ni jitihada za makusudi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt.




# Congo DRC yaziangukia Arsenal,Bayern Munich

SERIKALI ya Kongo imevitaka vilabu vya soka vya Arsenal, Bayern Munich na Paris St Germain kusitisha makubaliano yao ya udhamini ya utalii kwa Rwanda maarufu ''Vis_kiswahili imeripoti.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Therese Kayikwamba Wagner amevitaka Vilabu vya soka vya Arsenal, Bayern Munich na Paris St Germain kusitisha makubaliano yao ya udhamini ya utalii kwa Rwanda maarufu ''Visit Rwanda"kwa kile alichokiita kwamba ni ufadhili unaochangia umwagikaji wa damu katika mzozo mbaya wa kibinadamu nchini humo.

Waziri huyo ameviandikia barua vilabu hivyo vitatu wiki hii akielezea madhila wanayoyapitia watu wa mashariki mwa Kongo na kuhoji maadili ya mikataba yao ya ufadhili, akinukuu ripoti ya Umoja wa Mataifa iliyokadiria kuwa kuna Wanajeshi karibu 4,000 wa Rwanda wanaowasaidia Mgambo wa M23 nchini Congo.